*Mulika, Juz. 44(2), 153-171*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Uchunguzi wa Maumbo ya Wingi wa Heshima kwenye Kategoria za Kileksika za Lugha ya Kimatengo

*Fokas Nchimbi*[1]

DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na44t2.1

**Ikisiri**

Wingi wa heshima ni dhana ya kiisimujamii ambayo haijaelezwa vya kutosha kuhusu fasili na uwasilishwaji wake kwenye kategoria za kileksika katika lugha za Kibantu, ikijumuishwa lugha ya Kimatengo[2]. Aidha, kuna ukanganyifu wa kuchukulia wingi wa heshima kama dhana ya upole kwenye isimujamii za lugha za Kibantu. Lengo la makala hii ni kuchunguza uwasilishaji wa maumbo ya wingi wa heshima kwenye kategoria za kileksika yanayotumiwa kumrejelea mtu kwa heshima katika jamii ya Wamatengo kutegemeana na hadhi yake. Data za utafiti huu zilikusanywa kwa mbinu za usaili, majadiliano ya vikundi lengwa, na ushuhudiaji shiriki. Data hizo zilikusanywa kutoka kwa wazungumzaji wazawa wa Kimatengo waishio wilayani Mbinga, mkoani Ruvuma. Uchambuzi wa data umeongozwa na Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1987). Nadharia hii inaeleza kwamba, katika mazungumzo yoyote, kuna uwezekano kwa mzungumzaji kuonekana amemdhihaki au kumkejeli msikilizaji kwa aina ya maneno yanayotumiwa. Matokeo ya uchunguzi huu yanaonesha kuwa, katika Kimatengo, mofu za wingi wa heshima huwasilishwa kwenye kategoria za kileksika za nomino ({a}), viwakilishi ({a}, {b}), vivumishi ({a}) na vitenzi ({a}, {n}, {m}).

## 1.0 Utangulizi

Lengo mojawapo la matumizi ya lugha ni kuonesha, kuendeleza na kudumisha mahusiano, heshima na hadhi ya mtu katika jamiilugha (Lindström, 2022; Heim & Wiltschko, 2021). Matumizi hayo ya lugha katika jamiilugha yanaweza kuelezwa kwa kutumia dhana mbalimbali za kiisimujamii kama vile upole na wingi wa heshima. Wingi ni kategoria mojawapo ya kisarufi inayotumiwa katika lugha za binadamu kuwasilisha idadi ya wasemaji, watendaji na washiriki wengine wanaorejelewa katika tungo au muktadha wa mawasiliano.

---

[1] Mhadhiri, Idara ya Lugha na Fasihi, Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania, Baruapepe: fokasnchimbi@gmail.com, fokas.nchimbi@muce.ac.tz

[2] Kimatengo ni lugha ya Kibantu inayozungumzwa Kusini mwa Tanzania, Afrika Mashariki. Katika mgawanyo wa Guthrie wa lugha za Kibantu, lugha ya Kimatengo inaangukia katika kundi N13. Wazungumzaji wa Kimatengo wapatao 470,000 wanaishi katika eneo la milima la Kusini Magharibi mwa Tanzania katika maeneo ya kiutawala ya Wilaya ya Mbinga na katika baadhi ya maeneo ya kiutawala ya Wilaya ya Nyasa.

Kategoria ya kisarufi ya wingi inaweza kuwasilishwa katika lugha za Kibantu kupitia kategoria za kileksika za nomino, viwakilishi, vivumishi na vitenzi. Kategoria hii ya kisarufi ya wingi inaweza kutumiwa katika uchanganuzi na ufafanuzi wa kisarufi kwa kujidhihirisha kwa njia ya maumbo mbalimbali katika leksika za lugha. Moja ya vipengele vya kisarufi vinavyoweza kuchunguzwa na kufafanuliwa kwa matumizi ya kategoria ya kisarufi ya wingi ni dhana ya wingi wa heshima. Wingi wa heshima ni dhana inayohusu matumizi ya maumbo ya wingi katika kumrejelea mhusika mmoja ili kuashiria heshima. Matumizi ya maumbo kuashiria heshima yamedhihirika katika lugha mbalimbali za binadamu duniani, zikiwa ni pamoja na Kimatengo.

Dhana ya kiisimujamii ya wingi wa heshima inahusishwa na dhana nyingine ya upole kwa sababu, katika kuwasilisha maudhui ya heshima, huwasilishwa katika hali ya upole. Katika jamii, mtu mzima mwenye hadhi ya juu anapokuwa amekosea, kuna matumizi ya mofu za wingi zinazowasilisha urejeleaji wenye heshima kwa mkosaji huyo. Kwa hiyo, wingi wa heshima na upole ni vipengele sambamba vya isimujamii vinavyojitokeza katika baadhi ya lugha duniani, chimbuko lake likihusishwa na lugha kongwe ya Kilatini (Prou, 1910). Hata hivyo, jinsi dhana hiyo inavyojitokeza kwenye lugha za Kibantu, kama kilivyo Kimatengo, ni suala ambalo halijachunguzwa vya kutosha na ndiyo maana likachochea kufanyika kwa utafiti huu.

## 2.0 Mapitio ya Maandiko

Chimbuko la utumiaji wa nafsi ya wingi kueleza dhana ya heshima katika umoja limeelezwa kwa namna mbalimbali na kwa mikabala mikuu miwili: wingi wa heshima yaani ‘pluralis maiestatis’ na mkabala wa kihistoria (Maley, 1973; Hill, 2013). Mkabala wa ‘pluralis maiestatis’ unaotanabahisha asili na chimbuko la dhana ya maumbo ya wingi kubeba dhana ya heshima katika umoja ulianza mnamo karne ya tatu Kabla ya Kristo, ukitumika katika nyaraka za mawasiliano maalumu katika Ufalme wa Kirumi. Mwanaisimu Hofmann (1926) anaeleza kwamba Mfalme wa Kwanza wa Kirumi, anayejulikana kwa jina la Gordian wa III (238-244), alitumia dhana hiyo ya wingi kueleza dhana ya heshima katika umoja.

Mkabala wa pili ni ule wa kihistoria ambapo wanaisimu wanaeleza kwamba matukio mbalimbali ya kihistoria yalichangia kwa kiasi kikubwa kuwapo kwa matumizi ya wingi wa heshima katika lugha, hasa za kundi la Kihindi-Ulaya (Maley, 1973). Mfalme Diocletian wa Kirumi, aliyeingia madarakani mwaka 284 B.K., aligawanya madaraka ya ufalme wake mwaka 293 kwa wasaidizi wake ambao ni Chlorus na Galerius. Kwa kufanya hivyo, ndipo alipoanza kuwaita kwa nafsi ya wingi ‘vos’ *nyinyi* hata kama alikuwa akizungumza au kumhitaji mmojawapo. Maana ilikuwa kawaida kwa Warumi wa wakati ule kumwita mtu mmoja aliye katikati ya wengi au kundi la watu kwa nafsi ya wingi ‘vos’ *nyinyi* badala ya ile ya umoja ‘tu’ *wewe*. Hii ilifanyika ili kuonesha heshima. Kwa hiyo,

katika nyakati hizo, haikuwa rahisi kumwita mtu mmoja mwenye cheo aliye katikati ya wengi kwa nafsi ya umoja, kwa sababu kufanya hivyo kungetafsiriwa kuwa amedhihakiwa (Maley, 1973; Hill, 2013).

Matumizi ya wingi wa heshima si suala ibuka katika isimu mamboleo, bali yamekuwapo tangu karne nyingi zilizopita katika lugha za ulimwengu na kudhihirishwa kwa maandiko mbalimbali ya kale (Raynouard, 1816). Kwa mujibu wa Maley (1973), dhana hii inaonekana kuwa na chimbuko moja, yaani kutoka lugha ya Kilatini. Baadhi ya lugha za kundi la Kihindi-Ulaya ziliifanyia mabadiliko dhana hiyo kwa kuanzisha nafsi nyingine ya tatu ili kubeba dhana ya heshima kwa ajili ya nafsi ya pili. Kwa mfano, katika lugha ya Kihispaniola ‘usted-ustedse’ *wewe*, lugha ya Kireno ‘você-vocês’ *wewe* na lugha ya Kiitaliano ‘lei-loro’ *wewe* ni maumbo ya nafsi ya tatu yanayobeba dhana ya wingi wa heshima kwa nafsi ya pili (Maley 1973). Katika kundi hilo la lugha za Kihindi-Ulaya, Kifaransa hakikubadilika kwa kuanzishwa kwa nafsi ya tatu ibebayo dhana ya heshima, bali umbo la nafsi ya pili wingi lilitumika badala yake, kama ilivyokuwa asili ya matumizi hayo kutoka lugha ya Kilatini (Maley, 1973).

Kifaransa ni lugha mojawapo ya ulimwengu inayodhihirisha matumizi ya wingi wa heshima kurejelea watu kwa kutambua hadhi zao za kijamii kwa kutumia nafasi ya pili. Meng (2012) anaeleza kwamba matumizi ya maumbo ya wingi yanayochukua dhana ya umoja katika lugha ya Kifaransa yalisababishwa kwa kiasi kikubwa na dhana mbili muhimu: dhana ya itifaki na dhana ya mshikamano miongoni mwa wazungumzaji. Vilevile, Meng (2012) anaeleza kwamba matumizi ya nafsi ya wingi katika lugha ya Kifaransa huamuliwa na sababu mbalimbali za ndani na za nje baina ya wazungumzaji. Sababu hizo ni pamoja na mahusiano kati ya wazungumzaji, umri wao, hadhi na vyeo vyao. Hoja za Meng (2012) kuhusu lugha ya Kifaransa zinaonekana kushabihiana sana na zile zinazoibuliwa kupitia nadharia inayotumiwa katika utafiti huu, yaani Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1987).

Grand-Clément (1996) anatoa kanuni ya ujumla ya matumizi ya nafsi ya pili katika umoja na wingi wa heshima kwa kuzingatia mkabala wa mahusiano ya wazungumzaji tu. Ufafanuzi wake umejikita katika kufahamiana ama kutofahamiana baina ya wazungumzaji na mazoea baina yao. Hata hivyo, mkabala huu unaonekana kuwa na ughairi kwani, katika lugha ya Kifaransa, mtoto hawezi kutumia nafsi ya wingi wa heshima kwa yeyote wa nyumbani mwake au familia yake ili kuonesha heshima. Meng (2012) analeza kuwa tofauti hii inaweza kuchangiwa na mila na desturi za wahusika. Katika mazingira ya kijamii, wazungumzaji wa Kifaransa hulazimika kutumia nafsi ya wingi wa heshima kwa wateja wao ili kuonesha heshima na kutambua thamani yao, wasio na vyeo kwa wenye vyeo na wanafunzi kwa walimu wao (Meng, 2012).

Baadhi ya wanazuoni wanakizungumzia kigezo cha umri kuwa na nafasi kubwa katika kuamua matumizi ya nafsi ya wingi wa heshima katika lugha ya Kifaransa. Béal (1996), katika utafiti wake, anabainisha kwamba nafsi ya pili umoja hutumiwa zaidi miongoni mwa vijana wa umri chini ya miaka 25, huku kizazi kilicho na umri wa wastani wa miaka 50 mpaka 68 kikitumia zaidi nafsi ya pili umoja katika mazungumzo ya nyumbani, huku matumizi ya wingi wa heshima yakitamalaki katika mazingira rasmi.

Hali kadhalika, Kichina ni lugha mojawapo ulimwenguni inayodhihirisha matumizi ya maumbo ya wingi wa heshima kwa washiriki wa mazungumzo wanaochukuliwa kuwa watu wenye heshima na hadhi ya juu katika jamii. Meng (2012) anathibitisha kwamba katika lugha ya Kichina, matumizi ya nafsi ya heshima yanadhihirika; na wingi wa heshima umekuwa ukitumika mara nyingi. Meng anaeleza kwamba, katika jamii ya Kichina, nafsi ya heshima hutumiwa zaidi na wale wenye umri mdogo wanapozungumza na wakubwa wao kwa umri. Kwa upande mwingine, washiriki walio na umri mkubwa hutumia nafsi ya kawaida ya umoja au wingi wazungumzapo na wale walio na umri mdogo kuliko wao (Cao, 2007; Meng, 2012). Tofauti na lugha nyingine, Kichina hakitumii wingi ili kuonesha heshima bali hutumia nafsi maalumu '« 您 »' (Nín), ambayo hubeba dhana hiyo ya heshima (Hong, 1985; Lee, 2020; Cao, 2007; Hua, 2010). Nafsi ya heshima hutumiwa pia kwa mtu mwenye mamlaka, cheo au wadhifa mkubwa kuliko mzungumzaji mwenzake, licha ya kwamba mzungumzaji anaweza kuwa na umri mkubwa zaidi kuliko mshiriki wa mazungumzo mwenye cheo cha juu (Meng, 2012).

Katika baadhi ya lugha za Kibantu, kuna matumizi ya wingi unaoonesha heshima au hadhi ya mtu katika jamii. Utafiti wa Marten na Kula (2021) unaonesha kuwa licha ya kuwepo wingi wa heshima katika baadhi ya lugha za Kibantu, heshima huoneshwa zaidi katika majina ambapo mofu mahsusi hupachikwa kwenye nomino ili kuonesha heshima. Hii haiondoi ukweli kwamba kuna lugha chache za Kibantu zinazotumia maumbo ya wingi katika kubeba dhana ya upole na wingi wa heshima. Hivyo, Marten na Kula (2021) na Bentley na Kulemeka (2001) wanaeleza kwamba kuna lugha chache sana za Kibantu, kama vile Kichewa na Kizulu, zinazoweza kubeba wingi wa heshima. Hata hivyo, utafiti wao hautaji lugha ya Kimatengo kuwa miongoni mwa lugha zenye kaida hizo, suala ambalo lilichochea kufanyika kwa utafiti huu katika lugha ya Kimatengo.

Lugha ya Kichewa hutumia wingi ili kuonesha upole wa heshima unaotokana na umri na mamlaka ilhali umoja hutumiwa kati ya watu wenye rika moja au hutumiwa na mtu mwenye umri mkubwa azungumzapo na mtu mwenye umri mdogo (Bentley na Kulemeka, 2001; Marten na Kula, 2021). Katika lugha ya

Kizulu, kauli ya kutendwa hutumika kuonesha heshima (Poulos na Msimang, 1998).
Hali kadhalika, katika lugha ya Kiyao, hakuna umbo la wingi wa heshima, bali nafsi ya tatu umoja na wingi huweza kuonesha upole wa heshima. Katika lugha hiyo, nafsi ya pili wingi au umoja hazibebi heshima; badala yake, huonesha kejeli na dhihaka (Sanderson, 1922; Whiteley, 1966; Marten na Kula, 2021).

Katika matumizi ya lugha, ili mtu aweze kueleweka bayana, hupaswa kuzingatia kanuni zote za kisarufi, yakiwa ni pamoja na matumizi sahihi ya maumbo ya idadi (umoja na wingi) katika tungo. Hata hivyo, tafiti tangulizi zinaonesha kuwa wazungumzaji wa lugha mbalimbali hutumia maumbo ya wingi kumrejelea mtu mmoja, hasa wanapotaka kuashiria au kuonesha heshima kwa mlengwa (Maley, 1973; Bentley na Kulemeka, 2001; Hill, 2013; Marten na Kula, 2021). Kwa hiyo, utafiti huu ulichunguza mofolojia ya wingi wa heshima katika lugha ya Kimatengo. Lengo lilikuwa kubainisha mofu kwenye kategoria za kileksika zinazotumiwa kumrejelea mtu kwa heshima katika jamii ya Wamatengo kwa sababu ya hadhi yake.

## 3.0 Nadharia ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1987). Hii ni nadharia ya kipragmatiki na kiisimujamii inayofafanua jinsi wazungumzaji wanavyodumisha mahusiano katika mazungumzo kwa kutumia lugha. Nadharia hii imejengwa katika msingi wa USO uliobuniwa na Goffman (1967) unaorejelea taswira ya mtu binafsi katika mahusiano ya kijamii. Nadharia hii ina misingi mikuu mitatu: kwanza, USO una sura chanya na hasi. Sura chanya inahusu hulka ya binadamu ya kupenda kukubalika na kuheshimika. Sura hasi inahusu hulka ya binadamu ya kupenda kuwa na mamlaka na uhuru bila kuingiliwa. Pili, msingi wa nadharia hii ni kwamba, katika usemaji, kuna matendo uneni yanayotishia sura chanya na hasi za USO wa binadamu katika mahusiano ya kijamii. Matendo kama kuamrishwa, kupingwa na kutokubaliana ni mifano ya matendo yenye vitisho kwenye USO wa binadamu. Kutokana na vitisho hivyo, msingi wa tatu unaweka mkakati wa hatua za afua za kulinda sura chanya na hasi za USO wa binadamu katika mazungumzo. Kwa hiyo, msikilizaji anaweza kutumia maneno ya amri ili kujilinda dhidi ya kitisho kutoka kwa mzungumzaji. Matumizi ya lugha yanayoanza na maneno ya kumsifia msikilizaji kabla ya kumwomba afanye jambo ni miongoni mwa mikakati ya kupunguza matendo uneni yenye vitisho. Kuna uwezekano mkubwa mzungumzaji kuonekana amemdhihaki, kumkejeli au kumdharau msikilizaji kwa aina ya maneno anayotumia. Jambo hili linaweza kutokea kwa misingi ya kutoheshimu mahusiano kati yao (Salman na Betti, 2020; Hutabarat, 2021). Hivyo, matumizi ya wingi wa heshima katika lugha kama Kifaransa au Kimatengo, kwa kuzingatia mahusiano baina ya wazungumzaji, ni muhimu katika jamii za wazungumzaji wa lugha.

Kwa ujumla, Nadharia ya Upole inaeleza matumizi ya heshima katika mazungumzo ili kuepuka dhihaka, kuimarisha mshikamano na kudumisha mahusiano ya kijamii. Inahusisha viwango vya heshima vinavyotokana na mila, desturi na taratibu za kijamii, ambapo kushindwa kuizingatia kunaweza kuvuruga mawasiliano na kuvunja amani. Wanazuoni kama Brown na Levinson (1987) na Scollon na Scollon (1995) wanabainisha kuwa upole hujidhihirisha kupitia heshima, mshikamano na mamlaka, na hivyo kuathiri aina ya mazungumzo. Utafiti unaonesha kuwa upole huu unatokana na uhusiano wa kuheshimiana kati ya mzungumzaji na msikilizaji, na katika lugha nyingi, ikiwemo Kimatengo, wingi wa heshima unatumika kuonesha heshima kwa wenye mamlaka na kudumisha uhusiano bora.

## 4.0 Methodolojia ya Utafiti

Huu ni utafiti wa kitaamuli unaotumia mbinu ya maelezo. Data zilizotumika kuandika makala hii zilikusanywa katika vijiji vya Wilaya ya Mbinga iliyoko Kusini mwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Njia zilizotumika kukusanya data za utafiti huu ni usaili na majadiliano ya vikundi lengwa. Watoataarifa walikuwa wazungumzaji wazawa 21 wa lugha ya Kimatengo kutoka vijiji vitatu—Litembo, Wukiro na Mbuji—vilivyopatikana kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa. Mbinu hii ilikuwa faafu kwa sababu vijiji vya Litembo, Wukiro na Mbuji vinahusishwa na Wamatengo asilia wanaotofautiana na Wamatengo waliohamia baadaye katika vijiji vingine kama vile Tingi, Mpapa, Mkumbi, kwa kuvitaja baadhi tu (Ndunguru, 1972; Ebiner, 1985). Wazungumzaji walitoka katika vijiji hivyo vitatu ambapo kila kimoja kilikuwa na wazungumzaji saba (7), wakiwamo wanawake watatu na wanaume wanne. Mbinu ya usampulishaji taje ilikuwa mwafaka kwa kuwa mtafiti alilazimika kumpata mzungumzaji mmoja mwenye umri wa miaka zaidi ya 70. Baada ya kuzungumza naye, aliombwa kumtaja mzungumzaji mwingine anayeendana naye kiumri na mwenye uzoefu wa kutosha kuzungumza Kimatengo kisicho na mchanganyiko mkubwa wa lugha nyingine, hasa Kiswahili.

Mtafiti alifanya usaili na watu 11, na washiriki 10 waliobaki waligawanywa katika makundi mawili ya watu watanowatano kwa ajili ya majadiliano. Majadiliano ya vikundi lengwa yalikusudiwa kuhakiki data zilizotokana na usaili kuhusu wingi wa heshima unavyotumika katika lugha ya Kimatengo.

Vilevile, mtafiti alitumia mbinu ya ushuhudiaji shiriki. Hii ilimsaidia mtafiti kushiriki mazungumzo na watu mbalimbali wakiwa kwenye mikusanyiko ya sherehe za ngoma za asili zinazojulikana kama Kioda na Mganda. Kioda ni ngoma inayochezwa na wanawake wakati Mganda, kwa kiasi kikubwa ni ngoma inayochezwa na wanaume. Hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya mifumo ya kijamii na kuimarika kwa harakati za usawa wa kijinsia, ni kawaida kuwakuta wanawake wakicheza Mganda. Kinyume chake, haijawahi kushuhudiwa kwa

wanaume kucheza Kioda, isipokuwa kupiga ngoma ya Kioda kwa ajili ya wanawake. Mbinu hii ilimsadia mtafiti kulinganisha taarifa alizopata kwenye majadiliano ya vikundi lengwa na usaili na matumizi halisi ya lugha kwenye miktadha ya mikusanyiko ya kijamii. Orodha ya maumbo yaliyonukuliwa kutokana na usaili na majadiliano ya vikundi lengwa ilitumika kama mwongozo wa ushuhudiaji shiriki.

## 5.0 Matokeo ya Utafiti

Kwa mujibu wa Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson, wazungumzaji wa lugha huchagua maumbo na miundo ya lugha kwa kuzingatia aina na viwango vya mahusiano yaliyopo baina ya washiriki wa mazungumzo. Mathalani, matumizi ya lugha ya upole huamuliwa na mahusiano ya kuheshimiana yaliyopo baina ya wanajamiilugha husika. Uchambuzi wa data za utafiti huu unaonesha kuwa, katika lugha ya Kimatengo, wingi wa heshima unawasilishwa kwenye vipengele mbalimbali vya kileksika. Vipengele vya kileksika huambikwa mofu za wingi ili kuwasilisha dhana ya wingi wa heshima katika miundo ya kimofosintaksia ya lugha ya Kimatengo. Katika lugha ya Kimatengo, kategoria za kileksika zinazotumika kuwasilisha mofu za wingi wa heshima zinajumuisha nomino, viwakilishi, vivumishi na vitenzi kama vinavyofafanuliwa katika sehemu zinazofuata.

### 5.1 Maumbo ya Wingi wa Heshima kwenye Nomino za Kimatengo

Nomino ni kategoria ya kileksika inayotaja kitu, kiumbe, mahali, hali, dhana au tendo lolote liwalo (Kihore na wenzie, 2012). Uchambuzi wa data za utafiti huu unaonesha kuwa wingi wa heshima katika lugha ya Kimatengo huwakilishwa kwenye nomino kwa kutumia mofu mahususi. Mara nyingi, majina ya watu wenye hadhi ya juu hurejelewa kwa maumbo ya wingi katika mazungumzo. Majina binafsi ya watu yanaweza kutumiwa kuwasilisha wingi wa heshima katika lugha ya Kimatengo. Data Na. 1 inaonesha uwasilishaji wa wingi wa heshima kwa kutumia mofu {a}.

1.
(a) **A**songolo — Songolo
(b) **A**kigumi — Kigumi
(c) **A**kahundi — Kahundi
(d) **A**kilwambo — Kilwambo
(e) **A**bobis — Bobis
(f) **A**kapesa — Kapesa

**Chanzo**: Data za Utafiti (2024)

Katika data Na. 1(a)-(f), mofu ya wingi wa heshima {a} imeambikwa kwenye majina binafsi ya watu kuwasilisha hadhi ya juu ya watu wenye majina ‘Songolo’, ‘Kigumi’, ‘Kahundi’, ‘Kilwambo’, ‘Bobis’ na ‘Kapesa’. Kulingana na Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson, mofu {a} inatumika kwa upole katika lugha ya

Kimatengo ili kuonesha heshima kwa hadhi ya utu uzima au uzee wa watu wanaorejelewa. Katika umri wa utoto au ujana, majina hayo katika Kimatengo yanatajwa kama kawaida katika maumbo yake ya msingi 'Songolo', 'Kigumi', 'Kahundi', 'Kilwambo', 'Bobis' na 'Kapesa' pasipo kuambikwa mofu ya wingi {a}.

Hali kadhalika, wingi wa heshima unaweza kuwasilishwa kwa kutumia majina yanayoonesha shughuli za watu kama vile ukulima, uwindaji, uganga, ualimu na kadhalika. Uwasilishaji huo wa wingi wa heshima hudhihirika kwa matumizi ya mofu {a} inayojitokeza mwanzoni mwa majina hayo ya shughuli za watu za kiuchumi au kijamii kama inavyodhihirishwa na data Na 2.

2. (a) **a**sinyanga (*muuguzi*)
(b) **a**ganga (*mganga*)
(c) **a**bengi (*mwindaji*)
(d) **a**lemi (*mkulima*)
(e) **a**limi (*mfugaji*)
(f) **a**londa (*mlinzi*)
(g) **a**mwalimo (mwalimu)

**Chanzo**: Data za Utafiti (2024)

Katika data Na. 2(a)-(g), kuna matumizi ya mofu ya wingi {a} kuonesha urejeleaji wenye heshima kwenye majina ya watu wenye umri mkubwa au wazee katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Kwa msingi wa Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson, mofu {a} inatumika kwa upole katika lugha ya Kimatengo ili kuonesha hadhi ya utu uzima kwa watu wenye majina yanayoonesha ufanyaji wa shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Nomino hizo zote, yaani 2(a)-(g) zipo katika idadi ya wingi kwa kuambikwa mofu ya wingi wa heshima {a} na, hivyo, kuwa na maana ya wingi 'asinyanga' *wauguzi*, 'aganga' *waganga*, 'abengi' *wawindaji*, 'alemi' *wakulima*, 'alimi' *wafugaji*, na 'alonda' *walinzi*. Kwa mujibu wa Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson, wingi unaowasilishwa katika data hii si wingi wa kisarufi bali ni wingi wa heshima unaotokana na hadhi ya mtu katika jamii ya wazungumzaji wa lugha ya Kimatengo.

### 5.2 Maumbo ya Wingi wa Heshima kwenye Viwakilishi vya Kimatengo

Viwakilishi ni aina mojawapo ya maneno katika sarufi ya lugha yanayofanya kazi ya kuwakilisha nomino katika miktadha mbalimbali (Kihore na wenzie, 2012). Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kwamba viwakilishi huambikwa mwanzoni mwake mofu {a} inayoweza kutumiwa katika lugha ya Kimatengo kuonesha wingi wa heshima. Uwasilishwaji huo wa wingi wa heshima unaweza kuoneshwa kwa njia ya viwakilishi binafsi, viwakilishi kiima, na viwakilishi yambwa. Viwakilishi binafsi ni maneno yanayosimama badala ya nafsi ya kwanza, ya pili au ya tatu. Viwakilishi kiima ni viwakilishi nafsi vinavyotumika kama kiima cha sentensi; na

viwakilishi yambwa ni viwakilishi nafsi vinavyojitokeza kama yambwa kwenye muundo wa sentensi.

Data za utafiti huu zinaonesha kwamba mofu za wingi wa heshima hupachikwa kwenye viwakilishi nafsi kuwasilisha wingi wa heshima katika lugha ya Kimatengo kama inavyooneshwa na Data Na. 3.

3. (a) **m**wanonu (nyinyi)
   (b) **a**nonu (wao)

**Chanzo**: Data za Utafiti (2024)

Neno ‘mwanonu’ *nyinyi* katika data Na. 3(a) linawasilisha wingi wa heshima kwa ajili ya kiwakilishi nafsi cha nafsi ya pili umoja *wewe*. Mofu ya wingi wa heshima inayotumiwa kwenye muktadha huo ni {m}. Aidha, neno ‘anonu’ *wao* katika Data Na. 3(b) linawasilisha wingi wa heshima kwa ajili ya kiwakilishi cha nafsi ya tatu umoja *yeye*. Mofu ya wingi wa heshima inayotumiwa kuwasilisha dhana hiyo ni {a}. Matumizi ya mofu ya {a} ni njia ya upole ya kuonesha heshima wakati wa kumrejelea mtu mwenye umri wa utu uzima kama inavyoelezwa na misingi ya Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson.

Pia, mofu inayopachikwa kwenye viwakilishi kiima inaweza kutumiwa kuwasilisha dhana ya wingi wa heshima katika sentensi ya lugha ya Kimatengo kama inavyooneshwa na Data Na. 4.

4. (a) **M**we mwihika kilabo?
   *Wewe utakuja kesho*?
   (b) **B**ombi bihika kilabo.
   *Yeye atafika kesho*.

**Chanzo**: Data za Utafiti (2024)

Data Na. 4(a) na (b) inadhihirisha maumbo ya uwasilishaji wa wingi wa heshima ambapo mtu mmoja mwenye hadhi ya juu hurejelewa kwa mofu ya wingi nafsi ya pili {m}. Hali kadhalika, katika 4(b), mofolojia ya uwasilishaji wa wingi wa heshima imedhihirishwa ambapo mtu mmoja mwenye hadhi ya juu hurejelewa kwa mofu ya wingi nafsi ya tatu {b}. Kufuatana na misingi ya Nadharia ya Upole, matumizi ya mofu za wingi wa heshima hutokana na uhusiano wa kuheshimiana baina ya mzungumzaji na msikilizaji au mtu anayezungumziwa kama wanavyofafanua Marten na Kula (2021). Kuheshimiana huko kunatokana na hadhi ya msikilizaji au mzungumziwa kuwa ya juu kwa msingi wa umri au cheo.

Matumizi ya wingi wa heshima huweza kuwasilishwa kwa kutumia mofu zinazoambikwa kwenye viwakilishi kwa ajili ya nafsi ya pili na nafsi ya tatu. Data za utafiti huu zinadhihirisha kuwa wingi wa heshima hauwezi kuwasilishwa kwa

ajili ya nafsi ya kwanza inayozungumza na nafsi ya pili; au inayozungumza kuhusu nafsi ya tatu. Hata hivyo, katika nafsi ya kwanza, msemaji anaweza kutumia mofu ya wingi kwenye vipashio vya kileksika kwa lengo la kuonesha majigambo. Kwa mfano, ‘twe ngakutulapula’ *sisi hatuwezi kupigwa*, ‘twe ngakusindwa’ *sisi hatushindwi au* ‘twe ngakuhoba ndela’ *sisi hatuwezi kupotea njia*. Hii ni mifano ya majigambo anayoweza kufanya mzungumzaji wa lugha ya Kimatengo akitumia kiwakilishi cha wingi ‘twe’ *sisi* wakati akijirejelea yeye mwenyewe peke yake kwa kutumia nafsi ya kwanza wingi.

Hali kadhalika, kwa mujibu wa uchambuzi wa data za utafiti huu, mofu inayopachikwa kwenye viwakilishi yambwa huweza kuwasilisha dhana ya wingi wa heshima katika sentensi za lugha ya Kimatengo. Uwasilishaji wa mofu za wingi wa heshima kwenye viwakilishi vya Kimatengo unajitokeza katika Data Na. 5.

5. (a) Nunzalaki **m**we uwali.
   *Nakupikia wewe ugali*.
   (b) Tuntotulia **m**we hanzu.
   *Tulikuchukulia wewe kuni*.
   (c) Tumbutuki **m**we.
   *Tunakukimbilia wewe*.
   (d) Gualenda **b**ene.
   *Msubiri yeye mwenyewe*.
   (e) Gualalukia **b**ene.
   *Muulize yeye mwenyewe*.
   (f) Juatengila **b**ombi hanzu.
   *Alimfungia yeye kuni.*

   **Chanzo**: Data za Utafiti (2024)

Katika Data Na. 5(a)-(c), dhana ya wingi wa heshima imewasilishwa kwa matumizi ya mofu {m} inayojitokeza kwenye kiwakilishi ‘mwe’ *wewe* katika lugha ya Kimatengo. Hali kadhalika, katika Data Na. 5(d)-(e), dhana ya wingi wa heshima imewasilishwa kwa matumizi ya mofu {b} inayojitokeza kwenye kiwakilishi cha urejeshi ‘bene’ *yeye mwenyewe.* Data Na. 5(f) inaonesha kwamba dhana ya wingi wa heshima katika lugha ya Kimatengo inawasilishwa kwa mofu {b}inayoambikwa kwenye shina la kiwakilishi ‘-ombi’ *yeye.* Matumizi ya mofu {m} na {b} yanawasilisha kwa heshima na upole vitendo vinavyoelekezwa kwa watendewa au watendwa ambao ni watu wenye umri wa utu uzima au wenye vyeo katika jamii ya Wamatengo. Matumizi ya mofu za wingi wa heshima kwenye viwakilishi vya Kimatengo hutokana na misingi ya kuheshimiana baina ya mzungumzaji na msikilizaji au mtu anayezungumziwa kama inavyoelezwa kwenye Nadharia ya Upole.

**5.3 Maumbo ya Wingi wa Heshima kwenye Vivumishi vya Kimatengo**

Kivumishi ni neno linalotumiwa kueleza sifa za nomino kwa kutoa maelezo zaidi kuhusu nomino (Matinde, 2012). Kuna aina mbalimbali za vivumishi kama vile vivumishi vya sifa na vivumishi vimilikishi. Data za utafiti huu zinadhihirisha kuwa vivumishi vya sifa ni mojawapo ya kategoria ya kileksika inayotumiwa kuwasilisha mofu za dhana ya wingi wa heshima katika lugha ya Kimatengo. Dhana hii inawasilishwa katika Data Na. 6.

6. (a) Atate **a**kolongu
   *Baba mkubwa*
   (b) Amabo **a**kolongu
   *Mama mkubwa*
   (c) Ahoko **a**kolongo
   *Babu mkubwa*
   (d) Ambuja **a**kolongu
   *Bibi mkubwa*
   (e) Anijaja **a**kolongu
   *Mjomba mkubwa*
   (f) Anihenga **a**kolongu
   *Shangazi mkubwa*

   **Chanzo**: Data za Utafiti (2024)

Katika data Na. 6(a)-(d), dhana ya wingi wa heshima imewasilishwa kwa matumizi ya mofu {a} inayojitokeza kwenye kivumishi ‘kolongu’ *kubwa*. Kwa kuzingatia msingi wa kuheshimiana wa Nadharia ya Upole, mofu {a} inaweza kutumiwa kuwasilisha dhana ya wingi wa heshima kwenye kivumishi ‘kolongu’ cha lugha ya Kimatengo inapotumika mkabala na majina ya watu wenye hadhi ya juu katika ukoo. Kinyume chake ni kwamba mofu {a} haiwezi kutumiwa mkabala na majina ya watu wanaochukuliwa kuwa na hadhi ya chini.

Katika jamii ya Wamatengo, majina ya watu wanaochukuliwa kuwa wa hadhi ya chini, wakilinganishwa na watu wengine wenye hadhi ya juu, kama vile ‘mwana’ *mtoto, ‘*ndombu’ *dada*, ‘mbeli’ *kaka*, ‘nkosi’ *rafiki*, na ‘ndamu’ *shemeji*, hayawezi kuambikwa mofu {a} kwenye vivumishi vya Kimatengo ikiwa bado watu hao hawajafikia umri wa makamo au uzee. Majina hayo yanachukua mofu ya kawaida ya umoja kama inavyowasilishwa katika Data Na. 7.

7. (a) Ndombu **n**soku
   *Dada mdogo*
   (b) Mbeli **n**soku
   *Kaka mdogo*
   (c) Mwana **n**soku
   *Mtoto mdogo*

(d) Nkosi **n**soku
*Rafiki mdogo*
(e) Ndamu **n**soku
*Shemeji mdogo*

**Chanzo**: Data za Utafiti (2024)

Katika data Na. 7(a)-(d), kivumishi ‘soku’ *dogo* kinachukua mofu ya upatanishi wa kisarufi {n} ambayo ni mofu ya kawaida isiyowasilisha wingi wa heshima. Hii inamaanisha kuwa watu hao wanaorejelewa kwa matumizi ya majina ya ukoo hawana hadhi ya umakamo au uzee. Hata kama mmojawapo yeyote katika watu wanaotajwa kwenye orodha hiyo katika Data Na. 7 angekuwa mkubwa kwa rika lakini, bila kutimiza umri wa uzee au utu uzima, bado asingetumia mofu ya wingi wa heshima {a}. Badala yake, angetumia mofu ya umoja {n} kama katika ‘mbeli **n**kolongu’, yaani *kaka mkubwa*, kwa sababu mahusiano ya kuheshimiana yaliyopo baina ya wazungumzaji bado hayajafikia kiwango cha kuhitaji matumizi ya mofu ya wingi wa heshima.

**5.4 Maumbo ya Wingi wa Heshima kwenye Vitenzi vya kimatengo**

Data za utafiti huu zinaonesha kuwa, katika lugha ya Kimatengo, wingi wa heshima huwasilishwa kwa kutumia mofu zinazoambikwa kwenye vitenzi vikuu vya aina mbalimbali ambavyo hujumuisha vitenzi vya kutenda, vitenzi vya kuwa, na ruwaza ya vitenzi vya ‘kuwa na’. Katika lugha ya Kimatengo, mofu za wingi wa heshima kwenye vitenzi vya kutenda zinaweza kutumiwa na mzungumzaji anapomrejelea mtu katika nafsi ya pili na katika nafsi ya tatu. Katika nafsi ya pili, mofu zinazoambikwa kwenye kitenzi cha kutenda ni {n} na {m} kutegemeana na miunganiko na michakato ya kimofofonolojia katika lugha ya Kimatengo kama inavyowasilishwa katika Data Na. 8.

8. (a) Ambuja **n**tila ki?
*Bibi unatoroka nini?*
(b) Amabo **n**teliki ki?
*Mama umepika nini?*
(c) Ahoku **n**kalingi ki?
*Babu umekaanga nini?*
(d) **N**kotuka kuyoma !
*Usisikitike* !
(e) **N**kombi kunyumba.
*Tangulia nyumbani*.
(f ) **N**tela kulema.
*Lima kwa bidii*.
(g) **M**pala magambo!
*Unatafuta kesi!*
(h) **M**pahike.

*Umekosea.*
(i) **M**boka heno?
*Unaondoka sasa hivi?*
(j) **M**poliki ilombe?
*Umetwanga mahindi?*

**Chanzo**: Data za Utafiti (2024)

Katika data Na. 7(a)-(f), mofu {n} inajitokeza kwenye vitenzi vya kutenda 'tila' *toroka*, 'teleka' *pika*, 'kalanga' *kaanga* 'kotoka', *acha*, 'komba' *tangulia*, na 'tela' *kazana* kuwasilisha dhana ya wingi wa heshima katika lugha ya Kimatengo. Katika Data Na. 7(g)-(j), mofu {m} inajitokeza kwenye vitenzi vya kutenda 'pala' *tafuta*, 'boka' *ondoka*, na 'pola' *twanga* kuwasilisha dhana ya wingi wa heshima katika lugha ya Kimatengo.

Katika nafsi ya tatu mofu {a} huambikwa kwenye kitenzi cha kutenda kuwasilisha dhana ya wingi wa heshima katika lugha ya Kimatengo. Data Na. 8(a)-(e) zinadhihirisha maumbo ya wingi wa heshima kwenye vitenzi vya kutenda katika lugha ya Kimatengo.

8. (a) Atate **a**lema kwi lituhi.
*Baba analima shambani.*
(b) Amabu **a**hagula ngonde.
*Mama anachagua maharage.*
(c) Asongolo **a**huna ulei.
*Songolo anavuna ulezi.*
(d) Akigumi **a**gaba lituhi.
*Kigumi analima shamba.*
(e) Anakomba **a**loka uleli.
*Nakomba anasuka mkeka.*

**Chanzo**: Data za Utafiti (2024)

Data Na. 9(a)-(e) inawasilisha wingi wa heshima kwenye vitenzi vya kutenda '**a**lema', '**a**hagula', '**a**huna', '**a**gaba' na '**a**loka'. Mofu ya ngeli ya kwanza nafsi ya tatu wingi {a} imetumika kuwasilisha wingi wa heshima kwa nomino ambazo, kimsingi, zipo kwenye maana ya nafsi ya tatu umoja. Kwa mujibu wa Brown na Levinson (1987), Nadharia ya Upole inabeba dhana ya kiwango cha heshima kwa kuzingatia mahusiano, taratibu, mila na desturi miongoni mwa wazungumzaji lugha. Matumizi ya mofu ya wingi wa heshima {a} kwenye vitenzi vya kutenda katika Data Na. 9(a)-(e) yanajengwa na heshima inayotokana na mahusiano, taratibu, mila na desturi katika jamiilugha ya Wamatengo. Katika hali ya kawaida, mofu ya ngeli ya kwanza nafsi ya tatu {ju} ndiyo ingetumika kwenye upatanishi wa vitenzi kama inavyooneshwa katika Data Na. 10.

9. (a) Mwana **ju**lema kwilisamba.

*Mtoto analima shambani.*
(b) Mbomba **ju**hagula ngonde.
*Mwanamke anachagua maharage.*
(c) Songolo **ju**huna ulei.
*Songolo anavuna ulezi.*
(d) Kigumi **ju**gaba lituhi.
*Kigumi analima shamba.*
(e) Nakomba **ju**loka uleli.
*Nakomba anasuka mkeka.*

**Chanzo**: Data za Utafiti (2024)

Katika Data Na. 10(a)-(e), mofu ya kipatanishi cha kisarufi cha ngeli ya kwanza nafsi ya tatu umoja {ju} inatumika kwenye upatanishi wa vitenzi ‘julema’, ‘juhagula’, ‘juhuna’, ‘jugaba’ na ‘juloka’ kwa maana ya kipatanishi ngeli ya kwanza nafsi ya tatu umoja. Mbali na uwasilishwaji wa wingi wa heshima kwenye vitenzi vya kutenda, dhana hiyo inaweza kuwasilishwa kwenye vitenzi vya kuwa katika hali, hadhi au sifa fulani kama tunavyoweza kuona katika Data Na. 11.

10. (a) Akapinga **a**bi angukuna.
*Kapinga ni mshirikina*.
(b) Akapinga **a**bi atamu.
*Kapinga ni mgonjwa*.
(c) Akapinga **a**bi ahabi.
*Kapinga ni mchawi.*
(d) Mundu **a**bi mpala.
*Mtu ni mtundu.*
(e) Akigumi **a**bi alepi.
*Kigumi ni mlevi.*

**Chanzo**: Data za Utafiti (2024)

Katika Data Na. 11(a)-(e), mofu {a} imetumika kuwasilisha wingi wa heshima kwenye sentensi hizo za Kimatengo. Matumizi ya mofu hiyo yanamaanisha kuwa ‘Kapinga’, ‘mundu’ *mtu’* na ‘Kigumi’ wanaorejelewa ni watu wa makamo au wazee. Kama watu hao wanaorejelewa wangekuwa watoto au vijana, mofu ya upatanishi wa kisarufi kwenye kitenzi cha kuwa ‘-bi’ ingekuwa {ju} kama inavyooneshwa na Data Na. 12.

11. (a) Kapinga **ju**bi ngukuna.
*Kapinga ni mshirikina*.
(b) Kapinga **ju**bi ntamu.
*Kapinga ni mgonjwa*.
(c) Kapinga **ju**bi nhabi.
*Kapinga ni mchawi.*
(d) Mundu **ju**bi mpala.

*Mtu ni mtundu.*
(e) Kigumi **ju**bi ndepi.
*Kigumi ni mlevi.*

**Chanzo**: Data za Utafiti (2024)

Katika Data Na. 12(a)-(e), mofu {ju} inatumika katika sentensi hizo kama kipatanishi cha kisarufu cha ngeli ya kwanza nafsi ya tatu umoja. Mofu hiyo inamaanisha kuwa watu wanaorejelewa si watu wazima au wazee tofauti na mofu {a} katika data ya 11 inayoonesha kuwa wanaorejelewa ni watu wa makamo au wazee.

Hali kadhalika, matokeo ya utafiti huu yanadhihirisha kuwa Wamatengo hutumia mofu ya wingi wa heshima {a} wanapotaka kueleza uwepo katika mahali kwa watu wanaochukuliwa kuwa na hadhi ya juu katika jamii kama Data Na. 13 inavyoonesha.

12. (a) Akapinga **a**bi kunyumba.
*Kapinga yupo nyumbani.*
(b) Ahokomundu **a**bi kwilitui.
*Kapinga yupo shambani.*
(c) Akahundi **a**bi kunza.
*Kahundi yupo nje.*
(d) Mundu **a**bi mwikitengo.
*Mtu **yumo** kichakani.*
(e) Akigumi **a**bi kulosi.
*Kigumi yupo mtoni.*

**Chanzo**: Data za Utafiti (2024)

Katika sentensi za data Na. 13(a)-(e), mofu ya wingi wa heshima {a} imeambikwa kwenye shina la kitenzi cha kuwa mahali '-bi' *-wa* kuonesha hali au hadhi fulani katika jamii ya wazungumzaji wa lugha ya Kimatengo. Aidha, data za utafiti huu zinaonesha kuwa vitenzi vya 'kuwa na' katika lugha ya Kimatengo vinaweza kuwasilisha wingi wa heshima baina ya wazungumzaji. Ili kueleza kwamba mtu mwenye hadhi ya juu katika familia kama vile baba, mama, babu, bibi, mjomba na shangazi au mtu wa makamo au mzee katika jamii ya Wamatengo anamiliki kitu fulani, ni lazima kutumia kitenzi cha 'kuwa na' chenye mofu ya wingi wa heshima {a} kama inavyodhihirishwa na Data Na. 14.

13. (a) Atate **a**bi nu nkoha.
*Baba ana mkuki.*
(b) Amabo **a**bi ni ligela.
*Mama ana jembe.*
(c) Ambuja **a**bi nu uleli.
*Bibi ana mkeka.*

(d) Ahoku **a**bi nu mpeu.
*Babu ana fimbo ya kutembelea.*
(e) Akigumi **a**bi ni kiheneku.
*Kigumi ana ungo mdogo.*
(f) Akahundi **a**bi ni kilatu.
*Kahundi ana kiatu.*

**Chanzo**: Data za Utafiti (2024)

Katika data Na. 14(a)-(f), kuna uwasilishaji wa matumizi ya mofu ya wingi katika vitenzi vya 'kuwa na' yanayoonesha wingi wa heshima kwa watu wenye hadhi za juu katika familia na katika jamii kwa ujumla. Matumizi ya kitenzi cha kuwa na 'abi nu/ni' *ana*, katika 14(a)-(d), yanawasilisha mofu ya wingi wa heshima {a} kwa watu wenye hadhi ya juu kwenye ukoo ambao ni 'atate' *baba*, 'ambuja' *bibi,* na 'ahoku' *babu*. Katika matumizi ya kitenzi cha *kuwa na* 'abi ni' *ana*, katika 14(e) na (f), yanawasilishwa kwa mofu ya wingi wa heshima {a} kwenye majina binafsi ya watu wenye hadhi ya juu katika jamii, ambao ni 'Akigumi' na 'Akahundi' mtawalia. Kwa mujibu wa Brown na Levinson (1987), Nadharia ya Upole inabeba dhana ya kiwango cha heshima kwa kuzingatia mahusiano, taratibu, mila na desturi miongoni mwa wazungumzaji wa lugha. Matumizi ya mofu ya wingi wa heshima {a} kwenye vitenzi vya *kuwa na* katika data Na. 14(a)-(f) yanajengwa na heshima inayotokana na mahusiano, taratibu, mila na destusi katika jamii lugha ya Wamatengo.

Kwa muhtasari, Jedwali Na. 1 linaonesha kategoria za kileksika na mofu za wingi wa heshima zilizobainishwa na utafiti tulioufanya.

**Jedwali Na. 1: Muhtasari wa Mofu za Wingi wa Heshima kwenye Leksika za Kimatengo**

| | **Kategoria ya Kileksika** | **Mofu ya Wingi wa Heshima** |
|---|---|---|
| 1. | Nomino | {a} |
| 2. | Kiwakilishi | {a}, {b}, {m}, |
| 3. | Kivumishi | {a} |
| 4. | Kitenzi | {a}, {m}, {n} |

Jedwali Na.1 linaonesha kwamba, katika lugha ya Kimatengo, wingi wa heshima kwenye nomino unawasilishwa kwa mofu {a}, ambapo kwenye viwakilishi wingi wa heshima unawasilishwa kwa mofu {a}, {b} na {m}. Hali kadhalika, kwenye vipashio vya kileksika vya vivumishi, wingi wa heshima unawasilishwa kwa mofu ya wingi {a}. Kwenye vitenzi, vivyo hivyo wingi wa heshima unawasilishwa kwa mofu {a}, {m} na {n}.

## 6.0 Hitimisho na Mapendekezo

Katika utafiti huu, imedhihirika kuwa dhana ya wingi wa heshima inajitokeza kwenye mofosintaksia ya lugha ya Kimatengo. Katika lugha hiyo, mofu za wingi wa heshima hudhihirishwa kwenye kategoria mbalimbali za kileksika. Matokeo ya

utafiti huu yamedhihirisha kuwa kategoria za kileksika za Kimatengo zinazoambikwa mofu za wingi wa heshima ni nomino, viwakilishi, vivumishi na vitenzi kama inavyowasilishwa kwa muhtasari kwenye Jedwali Na. 1. Pia, matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa, tofauti na dhana ya upole, dhana ya heshima inayooneshwa kwenye mofosintaksia ya Kimatengo inaweza kuwasilishwa hata kama mtu anayerejelewa yuko mbali na mzungumzaji. Hii inadhihirisha kuwa suala la wingi wa heshima si suala la kuonesha wakati wote katika maneno ya upole unaoambatana na hali ya ukunjufu wa sura ya uso wa msemaji. Hii ndiyo sababu ya kwamba mofu za wingi wa heshima zinaweza kutumiwa kumrejelea mtu asiyekuwapo kwenye muktadha wa mazungumzo. Utafiti huu unapendekeza kufanyika kwa tafiti nyingine katika lugha ya Kimatengo ili kubaini vipengele vingine vya kiisimu vinavyoihusu lugha hiyo. Hali kadhalika, utafiti huu unapendekeza tafiti zaidi zifanyike katika lugha nyingine za Kibantu ili kufahamu kama kuna mifumo ya mofosintaksia ya uwasilishaji wa wingi wa heshima.

## Marejeleo


Béal, C. (1996). *Bonne intention, mauvaise impression nouvelle culture et lois de la politesse dans les interactions verbales entre Français et Australiens*, Thèse de Doctorat, Université Lyon 2.

Bentley, M. and A. Kulemeka (2001). *Chichewa*. Munich: Lincom.

Brown, L. (2015). Honorifics and politeness. *The handbook of Korean linguistics*, 303-319. University of Oregon: John Benjamins Publishing Company.

Brown, P. & Levinson, S. C. (1987). *Politeness: Some universals in language usage*. Cambridge University: Cambridge University Press.

Brown, R., & Gilman, A. (1960). The pronouns of power and solidarity. In T. A. Sebeok (Ed.), Style in Language (pp. 253–276). MIT Press.

Byon, A. S. (2006). The role of linguistic indirectness and honorifics in achieving linguistic politeness in Korean requests. https://doi.org/10.1515/PR.2006.013

Cao, X. (2007). The effect of age and gender on the choice of address forms in Chinese personal letters. *Journal of Sociolinguistics*, *11*(3), 392–407. https://doi.org/10.1111/J.1467-9841.2007.00329.X

Conlan, C. J. (2005). Face threatening acts, primary face threatening acts, and the management of discourse. *Broadening the horizon of linguistic politeness, Pragmatics & Beyond New Series (pp. 65Á83).* Amsterdam, Netherlands: John Benjamins Publishing Company.

Cook, M. (2019). *Address pronouns and alternatives*. The social dynamics of pronominal systems: A comparative approach, 304, 75. https://doi.org/10.1075/pbns.304.04coo

Fukada, A. & Asato, N. (2004). Universal politeness theory: application to the use of Japanese honorifics. *Journal of pragmatics*, *36*(11), 1991-2002. https://doi.org/10.1016/j.pragma.2003.11.006

Grand-Clément, O. (1996). *Savoir-vivre avec les Français - Que faire? Que dire?* Paris: Hachette.

Heim, J., & Wiltschko, M. (2021). *Acquiring the form and function of interactional language*. Paper presented at the annual meeting of the Linguistic Association of Great Britain and Northern Ireland (LAGB). https://aura.abdn.ac.uk/server/api/core/bitstreams/788e8019-1d9b-45f2-835f-df13637c0ee8/content

Hill, N. W. (2013). The emergence of the pluralis majestatis and the relative chronology of old Tibetan texts. International Institute for Tibetan and Buddhist Studies: GmbH.

Hobbs, P. (2003). The medium is the message: Politeness strategies in men's and women's voice mail messages. Journal of Pragmatics, 35, 243-262. https://doi.org/10.1016/S0378-2166(02)00100-5

Hofmann, J. B. (1926). *Lateinische Umgangssprache* (Vol. 17). Heidelberg, Germany: Carl Winter. https://catalog.hathitrust.org/Record/006229577

Hong, B. (1985). Politeness in Chinese: Impersonal pronouns and personal greetings. *Anthropological Linguistics*, *27*(2), 204-213. Trustees of Indiana University. https://www.jstor.org/stable/i30028059

Hua, Z. (2010). Language socialization and interculturality: Address terms in intergenerational talk in Chinese diasporic families. *Language and intercultural communication*, *10*(3), 189-205. https://doi.org/10.1080/14708470903348531

Hutabarat, N. M. P. (2021). Face threatening act of different ethnic speakers in communicative events of school context. *Pedagogika: Jurnal Ilmu-Ilmu Kependidikan*, *1*(1), 17-21. https://doi.org/10.57251/ped.v1i1.103

Kerbrat-Orecchioni, C. (2011). *L'impolitesse en interaction : aperçus théoriques et étude de cas. Studii şi cercetari filologice.* Seria limbi romanice, (09), 142-178. https://www.ceeol.com/search/article-detail?id=201625

Kihore, Y. M., Massamba, D. P. B., & Msanjila, Y. P. (2012). *Sarufi maumbo ya Kiswahili sanifu*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI.

Koo, J. (1995). *Politeness theory: universality and specificity*. Unpublished doctoral dissertation. Harvard University.

Lee, H. Y. (2020). Linguistic politeness in the Chinese language and culture. *Theory and Practice in Language Studies*, *10*(1), 1-9. 10(1), 1-9. http://dx.doi.org/10.17507/tpls.1001.01

Leech, G. N. (2005). Politeness: Is there an East-West divide? Journal of Foreign Languages, 6, 3-36. https://doi.org/10.1515/PR.2007.009

Lindström, J. K. (2022). Interactional linguistics. In *handbook of pragmatics* (pp. 795-801). John Benjamins Publishing Company. https://doi.org/10.1075/hop.m2.int11

Maley, C. A. (1973). The evolution of the French “Plural of Respect”. Romance Notes, 15(1), 188-192.

Marten, L., & Kula, N. (2021). *Expressing politeness and respect in Bantu languages: A comparative survey*. Centre for Advanced Studies of African Society (CASAS). https://doi.org/10.17159/casasv1i1.2021

Matinde, R. S. (2012) *Dafina ya Lugha: Isimu na Nadharia*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.

Meng, X. (2012). *Compétence en vouvoiement et en tutoiement dans la communication exolingue pour le français.* Synergies Chine, (7), 161-167.

Mgullu, R. S. (1999). *Fonetiki, fonolojia na mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Poulos, G. and C.T. Msimang (1998) *A linguistic analysis of Zulu*. Cape Town: Via Afrika.

Prou, M. (1910) *La politesse dans les langues modernes. Revue Universitaire*: éducation, enseignement, administration, préparation aux examens et concours, lettres et langues vivantes. Paris: Ecole de Chartes.

Raynouard, F. J. M. (1816) *Grammaire romane: Ou, Grammaire de la langue des troubadours*. (Vol. 1). Firmin Didot.

Sadeghoghli, H. & Niroomand, M. (2016) Theories on Politeness by Focusing on Brown and Levinson's Politeness Theory. *International Journal of Educational Investigations*, *3*(2), 26-39.

Salman, H. S. & Betti, M. J. (2020) Politeness and face threatening acts in Iraqi EFL learners’ conversations. Glossa, 3(8), 221-233.

Scollon, R. & Scollon, S.W. (1995) Intercultural communication: A discourse approach. Oxford: Blackwell.

Usami, M. (2006) Discourse politeness theory and cross-cultural pragmatics. *W:] Asako Yoshitomi, Tae Umino, Masashi Negishi (red.) Readings in second language pedagogy and second language acquisition: In Japanese context. Amsterdam: John Benjamins*, 19-42. https://doi.org/10.1075/ubli.4.05usa